BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Nne – Tarehe 15 Mei, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu kwa mwaka 2023/2024.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu kwa Mwaka 2023/2024.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

99. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kumekuwa na muingiliano wa madaraka na mgongano wa kimaslahi katika ukusanyaji wa taka na ada zinazohusiana na jambo hilo katika shehia huku Sheha akisimamia ukusanyaji wa taka katika shehia zikiwemo taka kutoka madukani na Manispaa nayo inakusanya ada za maduka zikiwemo ada za taka kutoka katika maduka ndani ya shehia.

(a) Je, ni upi utaratibu sahihi wa dhamana wa kukusanya taka katika shehia.

(b) Je, ni kwa nini Manispaa inadai ada za taka zilizokusanywa na shehia kutoka katika maduka ya ndani ya shehia.

(c) Je, ni mpango upi wa mgao wa ada hizo kati ya shehia na Manispaa zilizotokana na ada za taka za madukani katika shehia.

**<u>Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:</u>**

52. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Mabadiliko ya tabianchi ni moja kati ya changamoto za kidunia zinazoikabili Zanzibar katika maeneo mbali mbali ikiwa ni pamoja na eneo la Tumbe Bandarini.

(a) Je, kwa kiasi gani Serikali kupitia Wizara yako inalifahamu tatizo hilo.

(b) Je, Serikali kupitia Wizara yako ina mpango gani wa kulitatua tatizo hilo.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

39. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo,Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Wananchi wa jimbo la Nungwi kwa kiasi kikubwa wanategemea kilimo cha maweni kwa kulima mtama, mahindi, viazi vikuu na mazao mengine ya maweni. Mazao haya ili yavunwe vizuri yanahitaji mbolea ya samadi, lakini kuna changamoto kubwa kwa wakulima kuipata mbolea hiyo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia mbolea wakulima hawa.

**Wizara ya Afya:**

34. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kutokana na kuongezeka kwa hospitali za Wilaya na Mikoa.

(a) Je, Wizara haioni kuwa ipo haja ya kuwepo kwa daktari mkuu wa Serikali pamoja na madaktari wa mikoa (RMO).

(b) Je, ni nani anayewasemea madaktari kitaalamu na anayesimamia dhamana za madaktari hao katika kupangiwa Idara/Kitengo kutokana na taaluma (Profession) zao.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

117. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Ni jambo la kupongezwa kwamba Serikali, kupitia taasisi zake mbali mbali zikiwemo Manispaa, imekuwa ikipeleka na kudhamini watumishi wake kwenda kusoma sehemu mbali mbali ikiwemo nchi ya Uganda. Hata hivyo, inasikitisha na kutia wasiwasi kuona kwamba kuna wanafunzi waliopelekwa na taasisi za Serikali, wakiwemo wanawake, lakini Serikali haiwapatii posho za kujikimu kama ilivyokubalika kabla ya kwenda kusoma.

(a) Je, kwa sasa kuna wanafunzi wangapi kutoka Manispaa zetu waliopelekwa kusoma nchini Uganda ambao wanaendelea na masomo.

(b) Je, kiasi gani cha posho za kujikimu ambazo hawajalipwa wanafunzi hao hadi kufikia sasa.

(c) Je, ni lini Serikali itawapatia wanafunzi hao posho zao za kujikimu na kuwalipa madeni ya nyuma (arrears) hasa ukitilia maanani kuwa, wanafunzi hao wanasoma wakiwa ugenini na baadhi yao ni wanawake.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

13. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Serikali inatarajia kujenga barabara ya Wawi kwa Dkt. Omar Ali Juma kuiunganisha na barabara ya uwanja wa ndege kupitia skuli ya msingi Wawi.

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya ujenzi huo.

(b) Je, ni hatua gani zimefikiwa katika maandalizi ya ujenzi huo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

50. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa kumekuwepo na fursa nyingi za ajira kwa kazi ya kusomesha lugha ya Kiswahili nje ya nchi, huku Zanzibar ikiwa na vijana wengi waliohitimu vyuo vikuu na bado hawajapata ajira. Na kwa kuwa Serikali ina wajibu wa kuchangamkia fursa hii kwa kuwapa mafunzo ya muda vijana hao angalau ya miezi sita (6) ili wapate ujuzi zaidi wa kuifundisha lugha hiyo. Na kwa kuwa kuna umuhimu baada ya vijana hawa kupata ajira, Serikali ikafunga nao mkataba wa kupata asilimia fulani ya mshahara wao kwa mfano asilimia 10 zikaingia Serikalini kwa lengo la kuisaidia nchi yao kiuchumi.

Je, Serikali imechukua hatua gani mpaka sasa za kuhakikisha tunanufaika na fursa hizi za kuifundisha lugha ya Kiswahili nje ya nchi.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

81. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika shehia ya Mtangani kuna kisima cha maji ya bomba ambacho kilikuwa kinasambaza maji katika shehia hiyo kwa muda mrefu lakini kwa sasa maji hayo hayafiki vizuri tena. Tunapotaka kujua sababu za kutofika huko, huwa tunaambiwa kunasababishwa na tatizo la umeme kuwa mdogo.

(a) Je, kwa kiwango gani Mheshimiwa Waziri unalifahamu tatizo hili.

(b) Je, Mheshimiwa Waziri unatoa kauli gani kwa wanashehia ya Mtangani juu ya kadhia hii.

**<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>**

121. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kumekuwa na malalamiko mengi kwamba Serikali imekuwa ikitumia rasilimali za wananchi wa kawaida au makampuni yao kuimarisha maeneo na vivutio vya kihistoria, bila ya kuwalipa wananchi hao stahiki na ujira wao kama makubaliano yalivyofikiwa. Matengenezo ya dharura (urgent intervention) ya Bait el Ajab, matengenezo ya maeneo ya Mkamandume ya Pujini na maeneo ya kihistoria ya Mvuleni ni mfano wa hayo.

(a) Je, hadi kufikia Machi 2023, ni madeni yepi Serikali inadaiwa na watu na makampuni binafsi yanayotokana na uimarishaji wa maeneo na vivutio vya kihistoria Unguja na Pemba.

(b) Je, ni sababu zipi za kimkataba zinazoisababisha Serikali kutowalipa wananchi wa kawaida au makampuni yao yaliyotumika kuimarisha maeneo na vivutio vya kihistoria Unguja na Pemba.

(c) Je, ni lini Serikali itayalipa madeni hayo na kwa utaratibu upi.

**III. <u>HOJA ZA SERIKALI:</u>**

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu:</u>**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**15 Mei, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>**